Kadi ya Ripoti ya
Mkoa wa Manitoba

# Taarifa kwa Wazazi

DARASA LA 1 MPAKA 8



Manitoba

*Elimu ya Manitoba imezindua kadi ya ripoti ya kimkoa ya lazima kwa wanafunzi wa taaluma zote kuanzia mwaka wa shule 2013/2014.*

# Kwa Ujumla

## Kwa nini kuna kadi mpya ya ripoti?

Serikali ya Manitoba imezindua kadi mpya ya ripoti ya kimkoa kuboresha elimu Manitoba na kujenga ushirikiano mzuri kati ya wanafunzi, walimu wao na wazazi.

Hapo nyuma, kadi ya ripoti ilikuwa tofauti kwa kila darasa na, mifano mingine, kwa baadhi ya shule ndani ya madarasa sawa. Kadi mpya ya ripoti ya kimkoa itahakikisha kwamba wazazi wanapata taarifa sahihi mara kwa mara za namna watoto wao wanajifunza, hatua wanazojitahidi, ni hatua gani zitasaidia zaidi kujifunza na nini wanaweza kufanya kuwasaidia.

## Je, itakuwa rahisi kuielewa kadi ya ripoti?

Kadi ya ripoti inaandikwa kwa lugha nyepesi. Inakuambia uwezo wa mtoto wako na wapi mtoto wako anahitaji msaada. Kama una maswali kuhusu kadi ya ripoti, unaweza kuzungumza na mwalimu wa mtoto wako.

## Je, kadi ya ripoti ya taaluma ni sawa kwa madarasa yote?

Kuna mitindo mitatu ya kadi ya ripoti: moja ya Darasa la 1 mpaka 6, ya Darasa la 7 na 8 na nyingine ya Darasa la 9 mpaka la 12.

## Je, kutakuwa na maoni ya mwalimu kwenye kadi ya ripoti?

Ndiyo. Walimu wataandika maoni kuhusu kazi na tabia ya mtoto wako shuleni. Maoni yatakusaidia kutambua ni nini mtoto wako anafanya na msaada anahitaji wa kujifunza.

## Je, mtoto wangu anatathminiwa vipi?

Alama anazopata za kielemu zinaonesha jinsi mwanafunzi anavyofikia malengo ya mwongozo wa mtaala wa kusoma. Hii inajulikana kama vigezo vya alama vinavyoangaliwa. Alama anazopata mtoto wako haziwekwi kwa kulinganisha na za  wanafunzi wengine. Mambo kama mtazamo, juhudi na tabia zinaripotiwa kando na mafanikio ya kielimu. Huku ikieleweka kwamba vitu hivi vinaweza kuathiri matokeo ya kielimu na hivyo alama, kuviripoti kando husaidia kumpa mzazi habari ya ziada kuhusu uwezo wa mtoto wake na maeneo anafaa kuboresha.

Walimu hutoa njia nyingi za kuonesha ujuzi wao na kuelewa somo. Alama anazopata kwa ujumla zina akisi matokeo ya sasa na yanayoendelea ya kitaaluma. Kwa mfano, hii ina maana kwamba alama ya chini ya zoezi la mwanzo wa kufungua shule linaweza lisitiliwe mkazo katika kuamua alama za mtoto wako mwisho wa muhula kama baadaye alionesha mfululizo wa kujitahidi wa kuelewa zaidi au kupata ujuzi zaidi katika eneo hilo.

## Je mtoto wangu anaweza "kufeli" (kurudia) darasa?



Ndiyo. Uamuzi wa kumpitisha au kutompitisha mwanafunzi kunazingatia  tathmini makini wa mambo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na, miongoni mwa mambo mengine, ushahidi wa maendeleo ya mwanafunzi na ukuaji. Maamuzi ya kumpromoti yanatolewa na mkuu wa shule, ambaye anashauriana na walimu, wazazi na wataalamu wengine kama inavyotakiwa. Maamuzi ya kumwacha au kumpromoti mwanafunzi mara nyingi yanafanywa kwa faida ya mwanafunzi.

## Ni lini kadi ya ripoti itatumwa nyumbani?

Kadi ya ripoti inatumwa nyumbani wakati wa kipupwe (fall), wakati wa masika (spring) na mwisho wa mwaka wa shule.

## Je, nitapata taarifa kutoka kwa walimu wakati mwingine?

*Katika waraka huu, neno wazazi lina maanisha wazazi au walezi.*

Ndiyo. Kadi ya ripoti ni njia pekee ya kuwasiliana na wazazi. Njia nyingine ni pamoja na simu, barua pepe, ripoti ya maendeleo isiyo rasmi, mkutano wa wazazi na walimu, kongamano la wanafunzi na taarifa za habari za shule.

## Nifanye nini kama nina wasiwasi na utendaji wa mtoto wangu shuleni?

Ongea na mwalimu wa mtoto wako. Itakuwa ni jambo la busara kuorodhesha maeneo ambayo mtoto wako anapata shida. Muulize mwalimu ni namna gani mnaweza kufanyakazi pamoja kumsaidia mtoto wako.

# Programu za mwanafunzi

*Programming* ya mtoto wako inamaanisha kama mtoto wako anafuata mtaala kwa ngazi, au ngazi ya daraja la mitaala mahususi inayoonesha mahitaji yake ya kujifunza.

Kama mtoto wako hafuati alama za ngazi ya mtaala katika somo, kadi ya ripoti itaonesha ni ipi kati ya programu tatu zifuatazo zitumike.



### 1. IEP programming

"IEP" ina inarejelea mpango binafsi wa elimu. Mwanafunzi ambaye hatafikia malengo ya kujifunza ya alama kwa ngazi katika somo atakuwa na mpango binafsi wa elimu ambao utaelezea malengo yake binafsi ya kujifunza. Alama anazopata mwanafunzi huyu kwenye kadi ya ripoti inarejea malengo ya kujifunza kwa mwanafunzi huyo binafsi, na malengo hayo yanaelezewa wazi katika mpango wa mwanafunzi.

Kiashiria cha "IEP" kinaweza kutumika wakati mwanafunzi anafeli chini ya alama za darasani kwenye somo, na IEP ni sehemu ya hili. Kama hapo juu, alama anazopata mwanafunzi darasani kwenye kadi ya ripoti inaonesha malengo ya mwanafunzi ya kujifunza kama yalivyodokezwa kwenye mpango.

### 2. EAL programming

"EAL" ina rejerea Kiingereza kama nyongeza ya programming ya lugha. Mwanafunzi wa kwenye hatua ya kwanza ya kujifunza Kiingereza kama lugha ya ziada inalenga katika kujifunza Kiingereza katika eneo la somo hilo. Alama anazopata mwanafunzi huyu kwenye kadi ya ripoti inazingatia usawa wa lugha na malengo ya eneo la somo analojifunza kwa mwanafunzi huyo binafsi kwa kiwango cha lugha anayofahamu.

### 3. L programming

"L" inarejerea programming ya kujifunza Kifaransa, na inatumika katika programu ya *Français* pekee. Mwanafunzi ambaye anahitaji msaada zaidi wa kuendeleza ujuzi wa lugha ya Kifaransa anatakiwa kufuata mtaala wa mafanikio ya jimbo unaweza kuzingatia kujifunza Kifaransa katika mazingira ya eneo hilo la somo. Alama anazopata mwanafunzi huyu kwenye kadi ya ripoti inazingatia kwenye usawa wa lugha na malengo ya eneo la somo analojifunza kwa mwanafunzi huyo binafsi kwa kiwango cha lugha anayofahamu.

Katika mfano wa Darasa la 1 mpaka 6 kadi ya ripoti hapo chini, unaweza kuona ni aina gani ya programu inayohitajika kwa alama ya "x." Kama hamna kilichooneshwa, basi mtoto wako anafuata mtaala wa darasani wa malengo ya kujifunza. Hii ni pamoja na matukio ambapo mtoto wako ana marekebisho.

*Neno* marekebisho *linarejelea mabadiliko yaliyofanywa na mwalimu kama hatua, vifaa, mazoezi au bidhaa za mwanafunzi kumsaidia mwanafunzi kufikia malengo anayotarajia.*

| **Mathematics** | **Teacher:** | | | |
|---|---|---|---|---|
| ☐ **EAL** | ☒ **IEP** | Term 1 | Term 2 | Final |
| | Knowledge and understanding | | | |
| | Mental math and estimation | | | |
| | Problem solving | | | |
| Comments: | | | | |

*Programming* imeoneshwa hapa

# Mafanikio ya kielimu ya matarajio ya mkoa

## Darasa la 1 mpaka 6

Darasa la 1 mpaka 6, zifuatazo ni *alama za kipimo kuanzia 1 mpaka 4* zinatumika kwenye kadi ya ripoti kuonesha mafanikio ya kitaaluma ya mtoto wako kwa kila kategoria ya somo (imeelezewa hapo chini) kwa kila somo.

| Grade Scale | | Academic Achievement of Provincial Expectations |
|---|---|---|
| 4 | | Very good to excellent understanding and application of concepts and skills |
| 3 | | Good understanding and application of concepts and skills |
| 2 | | Basic understanding and application of concepts and skills |
| 1 | | Limited understanding and application of concepts and skills; see teacher comments |
| ND | | Does **N**ot yet **D**emonstrate the required understanding and application of concepts and skills; see teacher comments |
| Additional Codes | NA | **N**ot **A**pplicable |
| | IN | **In**complete: not enough evidence available to determine a grade at this time |

| One of the following codes is used if the expectations for a student are different from the grade-level curriculum in a subject. | |
|---|---|
| **EAL** (**E**nglish as an **A**dditional **L**anguage) | Achievement is based on expectations that focus on English language learning. |
| **IEP** (**I**ndividual **E**ducation **P**lan) | Achievement is based on expectations that reflect special learning needs. |

Hapo chini ni mfano kuanzia Darasa la 1 mpaka 6 kadi ya ripoti ya alama ya kipimo hiki kwa mwanafunzi anayechukua hesabu na programming ya EAL kwenye Term 2. Kumbuka kwamba kila kategoria ya somo inapokea alama yake binafsi kutoka kwenye kiwango.

| **Mathematics** | **Teacher:** | | | |
|---|---|---|---|---|
| ☒ **EAL** | ☐ **IEP** | Term 1 | Term 2 | Final |
| | Knowledge and understanding | 3 | 2 | |
| | Mental math and estimation | 2 | 3 | |
| | Problem solving | 3 | 3 | |
| Comments: | | | | |

Programming — Kategoria ya Somo — Muhula wa Sasa

## Kategoria ya somo

Kategoria ya somo ni maeneo ya maarifa na ujuzi katika kila somo mtoto wako anachukua shuleni. Wanakupatia uelewa mzuri wa namna mtoto wako anajifunza. Kategoria za masomo zinasaidia kuwaelewesha wazazi ni "nini" wanafunzi wanajifunza. Imetengenezwa kuwa sehemu ya kufundisha, kujifunza na kutathmini katika maeneo yote ya somo, sio tu kwa baadhi ya mada alizofundishwa.



# Mafanikio ya kitaaluma ya matarajio ya mkoa

## Darasa la 7 na 8

Darasa la 7 na 8, kwa kuongezea *alama za kiwango kuanzia 1 mpaka 4,* asilimia ya kipimo inatumika kutoa alama za jumla za somo. Hii inalenga kusaidia mpito wa shule kwenda sekondari kadi za ripoti  ambapo somo kwa ujumla linapewa kwa kila somo, kwa kutumia asilimia ya kipimo, kufupisha mafanikio ya mwanafunzi kulingana na alama wanazopata wanafunzi wanapokaribia kuhitimu. Jedwali lifuatalo linaonesha ni kwa namna gani alama za kipimo zinahusiana na zingine.



| Academic Achievement of Provincial Expectations | |
|---|---|
| **Grade Scale** | **Descriptor** |
| **4**<br>**80% to 100%** | Very good to excellent understanding and application of concepts and skills |
| **3**<br>**70% to 79%** | Good understanding and application of concepts and skills |
| **2**<br>**60% to 69%** | Basic understanding and application of concepts and skills |
| **1**<br>**50% to 59%** | Limited understanding and application of concepts and skills; see teacher comments |
| **ND**<br>**Less than 50%** | Does **N**ot yet **D**emonstrate the required understanding and application of concepts and skills; see teacher comments |

Mfano ufuatao kutoka darasa la 7 na 8 unaonesha kadi ya ripoti ya mwanafunzi anayesoma sayansi kwa alama za kawaida za kiwango cha alama za mitaala kwenye Term 2, na kategoria tatu ndani ya somo. Pia inaonesha tabia tatu za kujifunza, ambazo zimeelezewa kwa zaidi hapo chini.

| **Science** | | | | Teacher: | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ☐ **EAL** ☐ **IEP** | | | | ☐ **IEP** | | | |
| **Academic Achievement** | **Term 1** | **Term 2** | **Final** | **Learning Behaviours** | **Term 1** | **Term 2** | **Term 3** |
| Knowledge and understanding | 3 | 2 | | Personal management skills | U | U | |
| Scientific inquiry process | 3 | 3 | | Active participation in learning | C | U | |
| Design process and problem solving | 4 | 4 | | Social responsibility | S | C | |
| Overall grade | 78% | 70% | % | | | | |
| Comments: | | | | | | | |

Hizi ndizo *kategoria za somo*

Hii ndio *mienendo ya kujifunza*

# Mienendo ya kujifunza

Kwa kuongeza kuripoti mafanikio ya kitaaluma, kadi ya ripoti inaonesha jitihada za mtoto wako na tabia darasani, zinazoripotiwa chini ya “Mienendo ya Kujifunza,” kama zilivyoelezwa katika mfano kwenye ukurasa uliopita na chini.

Darasa la 1 mpaka 6, mienendo ya kujifunza inaripotiwa mara moja kwenye kadi ya ripoti ya mtoto wako (kwa masomo yote). Darasa la 7 na 8, inaripotiwa kwa kila somo analosoma mtoto wako. IEP itaonesha kama mtoto wako ana mpango binafsi wa elimu wenye malengo yanayohusiana na mienendo ya kujifunza.

| Learning Behaviours | |
|---|---|
| **Scale**<br>**C**: Consistently – almost all or all of the time<br>**U**: Usually – more than half of the time<br>**S**: Sometimes – less than half of the time<br>**R**: Rarely – almost never or never | |
| **Personal management skills** | Uses class time effectively; works independently; completes homework and assignments on time |
| **Active participation in learning** | Participates in class activities; self assesses; sets learning goals |
| **Social responsibility** | Works well with others; resolves conflicts appropriately; respects self, others and the environment; contributes in a positive way to communities |

Kwa wanafunzi katika Programu ya Kuzamishwa kwenye Kifaransa, pia kuna mienendo ya kujifunza kuhusu ushiriki wa wanafunzi katika kutumia Kifaransa.

Mienendo ya kujifunza haijajumuishwa moja kwa moja katika alama za mwanafunzi, lakini zinaweza kuathiri matokeo yao ya kitaaluma. Maendeleo chanya ya miendendo ya kujifunza yanaweza kusababisha mafanikio ya baadaye ya wanafunzi wakati wanaendelea na maisha yao kote ndani na nje ya shule. Kama wanafunzi wanafanya kazi kwa kujitegemea, huchukua hatua na kuheshimu maadili ya darasa, stadi hizi zinakwenda sehemu nyingine nyingi za maisha yao.



# Kwa taarifa zaidi

Tembelea tovuti ya Elimu ya Manitoba kwa taarifa zaidi kuhusu

- kile mtoto wako anajifunza kwenye **maeneo mbalimbali ya masomo:**
  www.edu.gov.mb.ca/k12/cur/parents/ (Programu ya Kiingereza)
  www.edu.gov.mb.ca/k12/cur/parents/fr_imm/ (Programu ya Kujifunza Kifaransa)
  www.edu.gov.mb.ca/m12/progetu/parents/ (Programu ya *Français*)
- sera na miongozo ya **tathmini ya mwanafunzi:**
  www.edu.gov.mb.ca/k12/assess/
- **Kadi ya Ripoti ya Taaluma:**
  www.edu.gov.mb.ca/k12/assess/report_cards/index.html

# Maoni yako yanakaribishwa

Uwe mzazi au mlezi, mwalimu, mwanafunzi au mwanajamii, maoni yako kwenye kadi ya ripoti mpya ni ya muhimu. Kwa ujumla, umeona hii kadi ya ripoti kuwa ya kuaeleweka na ya kukupasha taarifa? Kuna sehemu ya ripoti ambayo inaweza kuboreshwa zaidi?

Kama unataka kutoa maoni, tafadhali tuma barua kwenye anwani hapo chini au tembelea tovuti iliyotolewa hapo juu na jaza fomu na kutuma maoni yako sehemu ya kutoa maoni.

| Maoni kwenye Barua | Maoni kwenye Mtandao |
|---|---|
| *Provincial Report Card Feedback*<br>Manitoba Education<br>1567 Dublin Avenue<br>Winnipeg MB  R3E 3J5 | www.edu.gov.mb.ca/k12/assess/report_cards/feedback.html |